

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

05

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Muda: Saa 1:30

Mwaka 2018

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenyе jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.
3. Sehemu A ina alama **thelathini (30)** na sehemu B ina alama **ishirini (20)**

SEHEMU A (Alama 30)

1. Jibu kipengele (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku.
 - (i) Lipi ni kundi la viumbe hai pekee?
 - a) Jani, ndege na jiwe
 - b) Paka, mti na kuku
 - c) Mti, jani na mbao
 - d) Kiti, jani na ndege []
 - (ii) Gesi ya oksijeni inasaidia kuunguza chakula ili kupata.
 - a) Nishati
 - b) Moshi
 - c) mvuke
 - d) hewa []
 - (iii) Kwanini ni mhimu kusafisha miili yetu?
 - a) Ili kuzuzia magonjwa
 - b) Ili kupaka mafuta
 - c) Ili kupendezesha ngozi
 - d) Ili kuupa mwili hewa []
 - (iv) Yapi ni madhara ya uharibifu wa mazingira?
 - a) Kupotea kwa wadudu
 - b) Kusambaa kwa mavumbi
 - c) Kuongezeka kwa wanyama
 - d) Kutoke kwa magonjwa []
 - (v) Maji yana umuhimu gani kwa viumbe hai?
 - a) Kusafirisha virutubisho
 - b) Kutengeneza chakula
 - c) Kuyeyusha virutubisho
 - d) Kutuliza kiu []
2. Jibu vipengele (i) – (ii) kwa kuoanisha maelezo kuhusu sehemu za runinga katika orodha A na sehemu za runinga katika orodha B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

Orodha A	Jibu	Orodha B
(i) Sehemu inayoonesha picha na maandishi kwenye runinga.	[]	A. Rimoti
(ii) Sehemu inayotoa sauti kwenye runinga ili kupata ujumbe.	[]	B. Vitufe
(iii) Sehemu ya kuamrishia runinga kwa mbali.	[]	C. Swichi
(iv) Sehemu inayodaka mawimbi ya runinga angani.	[]	D. Waya
(v) Sehemu inayosafirisha umeme kutoka kwenye soketi hadi kwenye runinga.	[]	E. Spika
		F. Antenna
		G. sikrini

3. Jibu kipengele (i) – (v) kwa kuchagua neno sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika kwenye nafasi uliyopewa.

Chaja, laini ya simu, sikrini, antenna, kipaza sauti, betri

- (i) Sehemu gani hutumika kuonesha majina na namba kwenye simu?
- (ii) Sehemu inayopokea mawimbi ya sauti na picha inajulikana kama _____
- (iii) Sehemu inayoingiza nguvu ya umeme kwenye simu inaitwaje?
- (iv) Sehemu gani inahifadhi nishati ya umeme kwenye simu?
- (v) Sehemu gani hutumika kuunganisha simu za mtandao wa simu?

SEHEMU B (Alama 20)

4. Umepewa hatua A – E za ufuaji wa soksi. Panga hatua hizo kwa mtiririko kuanzia hatua ya kwanza hadi ya mwisho kwa kuandika sentensi ya hatua husika katika nafasi ya kujibia uliyopewa.

- A. Zisuuze soksi katika maji safi kuondoa sabuni.
- B. Fikicha sehemu za juu na chini za soksi.
- C. Anika soksi kwenye Kamba ili zikauke.
- D. Ziweke soksi kwenye beseni la maji safi na pakaa sabuni.
- E. Andaa maji safi na sabuni.

Majibu:

Hatua	Herufi
Hatua ya 1	
Hatua ya 2	
Hatua ya 3	
Hatua ya 4	
Hatua ya 5	

5. Chunguza picha zifuatazao kisha jibu maswali katika kipengele (i) – (v)



- (i) Taja shughuli inayofanywa na watu wawili wanaolea kwenye maji.
- (ii) Tofauti na binadamu, ni mnyama gani mwengine anaelea kwenye maji?
- (iii) Ni ugonjwa gani anaweza kuenezwa na mnyama anayeelea katika maji?
- (iv) Taja dalili mbili (2) za ugonjwa ulioutaja
- (v) Ogani gani za mwili hushambuliwa na ugonjwa huo?